**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU USIMAMIZI NA UDHIBITI WA TAKA HATARISHI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ndugu January Makamba (Mb.), akiongozana na Dkt. Samwel Gwamaka Mafwenga, Mkurugenzi Mkuu na maafisa waandamizi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, jana tarehe 22 Machi 2019, ametembelea Bandari ya Dar es Salaam na kutoa maelekezo na maagizo kadhaa kuhusu utaratibu wa biashara ya taka hatarishi/zenye madhara (harzadous waste).

Ofisi ya Makamu wa Rais imepewa mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira nchini kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 na Kanuni zake. Aidha, usimamizi na udhibiti wa taka zenye madhara umebainishwa kwenye Vifungu vya 133 -139 vya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Pia Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Usimamizi na Udhibiti wa Taka za Sumu) za Mwaka 2009 zimetoa miongozo ya kudhibiti taka sumu hapa nchini pamoja na mambo mengine yahusuyo uhifadhi wa mazingira.

Taka hatarishi (zenye madhara) ni pamoja na vyuma chakavu, taka za kieletroniki, dutu hatarishi, mafuta machafu, taka za hospitali, Betri zilizotumika na aina ya taka zote zinazotoka migodini. Taka hizi hatarishi zinaweza kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu, viumbe hai na mazingira. Ili kuzuia na kudhibiti athari mbaya zitokanazo na taka zenye madhara, mfumo mahsusi unaofanya kazi kwa ufanisi wa kudhibiti taka hizi unapaswa ufuatwe kama ulivyobainishwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Usimamizi na Udhibiti wa Taka za Sumu) za Mwaka 2009.

Katika miezi ya hivi karibuni, imebainika uwepo wa ukiukwaji wa Sheria na Kanuni zinazosimamia na kudhibiti taka zenye madhara nchini na mkataba wa kimataifa wa Basel unaohusu udhibiti wa usafirishaji wa taka zenye madhara na taka nyingine baina ya nchi na nchi ambao Tanzania ni mwanachama. Ukiukwaji huo unahusisha ukusanyaji, usafirishaji na urejeleshaji wa taka zenye madhara. Kutokana na hali hii, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mamlaka aliyopewa kwenye Sheria ya Mazingira, ametoa maagizo yafuatayo:

1. Watu wote wanaojihusisha na biashara ya Uingizaji Nchini (importation) na Usafirishaji Nje ya Nchi (exportation) wa taka zenye madhara, ikiwemo vyuma chakavu, betri zilizotumika na taka za kielektroniki, wanaarifiwa kuwa biashara hiyo imesimamishwa kwa sasa hadi uhakiki wa vibali vilivyotolewa na mamlaka mbalimbali utakapofanyika

na hadi utaratibu madhubuti wa udhibiti utakapowekwa ndani ya kipindi cha wiki tatu kuanzia sasa.

2. Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kifungu cha 133(1) kinasema “itakuwa ni kosa kuingiza au kusafirisha nje ya Tanzania taka zenye madhara bila kuwa na kibali kilichotolewa na Waziri”. Vilevile, kifungu cha 133(2) kinasema “mtu yoyote hataruhusiwa kusafirisha taka zenye madhara ndani ya nchi au kupitia Tanzania bila kupewa kibali kutoka kwa Waziri [mwenye dhamana ya Mazingira]”. Kwa msingi huo, vibali vyote vya kukusanya na kusafirisha taka hatarishi (ndani na nje ya nchi) vilivyotolewa na mamlaka nyingine havitoshelezi kufanya biashara hii bila kibali kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Mazingira.

3. Watu wote wanaojihusisha na biashara ya ukusanyaji, usafirishaji au urejerezaji wa vyuma chakavu, taka za kieletroniki, taka za kemikali, mafuta machafu, taka zitokanazo na huduma za afya na betri zilizotumika watatakiwa kuanzia sasa kwenda kujiandikisha upya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, na kuhakikiwa uhalali wa vibali vyao na uwezo wao wa kuendelea na shughuli hizo na baada ya hapo kutolewa vibali upya kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais kwa utaratibu mpya. Uhakiki huu unaanza sasa na utamalizika ndani ya wiki mbili. Baada ya hapo yoyote anayefanya shughuli hizi bila kibali kipya atachukuliwa hatua kazi za kisheria.

4. Ofisi ya Makamu wa Rais inaandaa mkutano wa wadau wa sekta za umma tarehe 22 Machi, 2019 utakaofanyika Dodoma na baadaye mkutano kati ya Serikali na wadau wa sekta binafsi ili kukubaliana njia bora za usimamizi na udhibiti wa taka zenye madhara.

5. Ofisi ya Makamu wa Rais inatarajia kufanya mabadiliko Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Usimamizi na Udhibiti wa Taka za Sumu) za Mwaka 2009 pamoja na kuandika kanuni mpya za udhibii wa taka za kielektoniki ili kuweka udhibiti bora zaidi.

6. Wafanyabiashara wanaojihusisha na ukusanyaji, usafirishaji na urejereshaji wa taka hatarishi wanatakiwa kutokupokea taka hizo kutoka kwa mtu yeyote asiyekuwa na kibali kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.

7. Kuna makonteina 44 ya vyuma chakavu katika Bandari ya Dar es Salaam ambayo yalikuwa kwenye hatua za mwisho kwenda nchini India bila kuwa na vibali husika. Pamoja na makontena hayo kuzuiliwa kwa barua kabla ya ziara ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, makontena 34 yalisafirishwa katika mazingira yasiyoeleweka. Kwa msingi huo, Waziri Makamba ameagiza mambo yafuatayo:-

    a) TAKUKURU pamoja na mamlaka nyingine husika wafanye uchunguzi wa mazingira ya kusafirishwa kwa kontena 34 hata baada ya wahusika wote kupata taarifa ya kuzuiwa.

    b) Mamlaka ya Bandari, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Tume ya Madini wawezeshe uchukuaji wa sampuli ya vyuma chakavu katika makontena yaliyobaki kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara ili kubaini iwapo hakuna bidhaa za ziada katika mizigo hiyo au vyuma hivyo.

c) Mwenye mzigo na wakala wake wanatakiwa kuwajibishwa kwa kosa la kutaka kusafirisha mzigo huo bila kuwa na vibali stahiki.

d) Makontena yaliyobaki yaendelee kuzuiliwa hadi hapo hadi uchunguzi wa kimaabara utakapokamilika na taratibu stahiki zitakapofuatwa.

e) Kule makontena yanapopelekwa wajulishwe kwamba wasafirishaji wamekiuka utaratibu.

8. Vilevile, imebainika kuwepo mzigo wa vyuma chakavu ulioingizwa kama “loose cargo” kwenye majahazi ukitokea Zanzibar. Mzigo huo pia unazuiwa hadi uchunguzi wa mazingira ya kuingizwa kwake utakapokamilika. Wahusika pia watachukuliwa hatua kwa kuingiza mzigo huo bila kufuata taratibu.

9. Mwisho, Ofisi ya Makamu wa Rais inatoa wito kwa wananchi wote kuwa mtu yeyote atakayejihusisha na ununuaji au uuzaji wa vyuma chakavu vinavyotokana na muindombinu ya taifa atashitakiwa kwa kosa la uharibifu wa miundombinu chini ya sheria za uhujumu uchumi.

10. Tunawasihi wananchi wote pia kutoa taarifa haraka kwa mamlaka husika, ikiwemo NEMC na Ofisi ya Makamu wa Rais, pale wanapohisi au kuona mtu au kampuni yoyote inaingiza nchini taka za aina yoyote kutoka nje ya nchi au ukusanyaji wa vyuma chakavu, taka za kieletroniki na betri zilizotumika na utupaji wa taka za hospitali unafanyika kinyume na utaratibu.

IMETOLEWA NA OFISI YA MAKAMU WA RAIS
22 MACHI 2019